MAELEZO YA MWENYEKITI WA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI KWA WAANDISHI WA HABARI KUHUSU TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA ZOEZI LA MAJARIBIO (PILOT) LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KWA KUTUMIA MFUMO WA BVR

JIJINI DAE ES SALAAM TAREHE 30/12/2014.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Watendaji wa Tume,

Mabibi na Mabwana.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi, napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisheni kwa mara nyingine katika Mkutano huu muhimu wa kupeana taarifa kuhusu tathmini ya Utekelezaji wa zoezi la Majaribio (pilot) la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutumia mfumo wa Biometric Voters Registration (BVR) lililofanyika hivi karibuni katika kata tatu za Kawe mkoani Dar es salaam, Kilombero mkoani Morogoro na Mlele mkoani Katavi.

Pamoja na majukumu mengi mliyo nayo, lakini mmeweza kuupa umuhimu wa pekee mkutano wetu huu na kuhudhuria kwa kiwango kikubwa hivyo kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi nasema Ahsanteni na Karibuni sana.

Ndugu Wanahabari,

Kama nilivyosema, Tume inakutana nanyi ili kuwapa taarifa kuhusu Tathmini ya Utekelezaji wa zoezi la Majaribio la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililofanyika kwa siku 7 katika Kata za Bunju na Mbweni zilizopo Jimbo la Kawe katika Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es salaam, Kata za Ifakara, Kakingiuka, Ipangala, Mlabani na Viwanja Sitini zilizopo katika Jimbo la Kilombero Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro na Kata za Ikuba, Usevya na Kibaoni katika Halmashauri ya Mlele mkoani Katavi.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi hivi karibuni iliendesha zoezi la Majaribio *(PILOT)* la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutumia teknolojia ya Biometric yaani Biometric Voters Registration (BVR). Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuzingatia kwamba ilikuwa inatambulisha

matumizi ya teknolojia mpya katika Uandikishaji Wapiga Kura iliona ni vema ikaanza na zoezi dogo la majaribio ambalo kimsingi ndilo lingekuwa dira na kielelezo cha kule tunakoelekea yaani Uandikishaji wa Wapiga Kura nchi nzima utakaoanza mwezi February 2015.

Zoezi la hilo la Uboreshaji wa Majaribio kwa majimbo hayo matatu lilipangwa kuanza tarehe 15/12/2014 na kufanyika kwa siku saba ingawa kutokana na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zoezi hilo lilianza kwa tarehe tofauti. Jimbo la Kawe zoezi lilianza tarehe 16 na kumalizika tarehe 22/12. Halmashauri ya Kilombero zoezi lilianza tarehe 15/12/2014 na kumalizika tarehe 21/12/2014 na katika halmashauri ya Mlele zoezi lilianza tarehe 17/12/2014 hadi tarehe 23/12/2014. Jumla ya BVR KITS 250 zilitumika katika Uboreshaji huo kwa mchanganuo ufuatao: Halmashauri ya Kilombero Kits 80, Halmashauri ya Mlele Kits 80 na Halmashauri ya Kinondoni Kits 90. Vituo katika Kata zote vilikuwa vinafunguliwa saa 2.00 asubuhi na kufungwa saa 12.00 jioni.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Tume inapenda kuwafahamisha kuwa zoezi hilo la Majaribio *(PILOT)* la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika majimbo matatu yaliyotajwa limefanyika na kukamilika kwa mafanikio makubwa licha ya changamoto za hapa na pale zilizojitokeza.

Tunasema mafanikio makubwa kwa sababu matokeo ya jumla yanaonyesha kuwa idadi ya waliojiandikisha imevuka malengo. *(need comparison figures)*

Mkoa wa Dar es salaam, Kata za Bunju na Mbweni Wapiga Kura 15,123. Mkoa wa Morogoro Kata za Ifakara, Kakingiuka, Ipangala, Mlabani na Viwanja Sitini Wapiga Kura 19,188 na Mkoa wa Katavu Halmashauri ya Mlele kata za Ikuba, Usevya na Kibaoni Wapiga Kura 11,210.

Pamoja na mafanikio hayo napenda nikiri kuwa zilikuwepo changamoto kadhaa wakati wa utekelezaji wa zoezi hilo. Changamoto hizo zinaweza kuwekwa katika makundi makubwa manne kama ifuatavyo: Matatizo yaliyotokana na 'Settings' za BVR Kits, Matatizo yaliyosababishwa na Software na Matatizo ya hardware na mwisho matatizo ya fedha na lojistiki.

Mbali ya changamoto hizo zilikuwepo pia changamoto nyingine za kimiundombinu na kibinadamu. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na ile ya Hali ya Hewa hususan katika jiji la Dar es salaam na Morogoro. Nadhani mtakubaliana nami kuwa pamoja na kuwa jiji la Dar es salaam kwa kawaida lina hali ya hewa ya joto lakini kwa takribani mwezi mmoja hivi uliopita kumekuwa na ongezeko la joto hali iliyosababisha hata baadhi ya vifaa vya kuandikishia hususan 'BVR Kits' wakati mwingine kushindwa kufanya kazi inavyotakiwa na hivyo kusababisha shughuli za uchapishaji wa Kadi za Kupigia Kura kuchelewa.

(Hali ya joto ndani ya madarasa nje nako upigaji picha unakuwa mgumu kutokana na mwanga)

Aidha ushirikiano mdogo kutoka kwa Wananchi nao ulikuwa changamoto iliyosababisha zoezi hilo kwenda taratibu. Baadhi ya wananchi kushindwa kuzingatia maelekezo yaliyokuwa yakitolewa na BVR Operators kutokana na uelewa duni kwani ilibainika pia kuwa bado kuna idadi kubwa ya wasiojua Kusoma na Kuandika hali iliyofanya zoezi la Uchukuaji wa alama za Vidole (Fingerprint) na Utiaji wa Saini kuwa mgumu.

Kadhalika kumekuwepo na mwamko mkubwa kwa wananchi kujitokeza kwa wingi ili kujiandikisha. Hata hivyo Tume bado inafanya utafiti ili kubaini kama kweli idadi hiyo kubwa ya wanaojiandikisha ni wapiga Kura au ni kwa madhumuni ya kupata Kadi ya Kupigia Kura kwa ajili ya matumizi mengine.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Ni vyema ieleweke wazi kuwa kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na kwa ajili ya Kura ya Maoni ya Katiba Mpya, Mpiga Kura atatumia Kitambulisho cha Mpiga Kura alichopatiwa na Tume baada ya kuandikishwa katika mfumo huu tu na si vinginevyo. Vitambulisho vilivyotolewa katika uboreshaji huu wa majaribio ni vitambulisho halisi hivyo kila aliyejiandikisha katika zoezi hili la majaribio ni muhimu atunze kadi yake kwa ajili ya matumizi yaliyotajwa kwa kuwa taarifa zake tayari zimeingia katika Kanzi data ya Tume hivyo hataweza tena kujiandikisha kwa mara nyingine hata kama atabadilisha kituo cha kujiandikishia.

Ndugu zangu Wanahabari,

Ni muhimu wananchi wakapata taarifa hizi kwa usahihi kwa vile wapo baadhi ya Watu waliodhani kuwa kwa kuwa hilo lilikuwa ni zoezi la majaribio basi watakuwa na fursa nyingine ya kujiandikisha wakati wa zoezi la nchi nzima. Napenda nisisitize hapa kuwa kwa yeyote aliyejiandikisha katika zoezi hili hataweza tena kujiandikisha labda tu kwa yule ambaye atahitaji kubadilisha taarifa zake kutokana na sababu kama zilivyofafanuliwa na Tume.

Itakumbukwa kwamba Tume ilipoanza kuelezea nia yake ya kutumia teknolojia ya Biometric Voters Registration (BVR) na kuachana na mfumo wa zamani wa Optical Mark Recognition katika uandikishaji wa Wapiga Kura tulieleza kuwa miongoni mwa sababu zilizoisukuma Tume kufikia hatua hiyo ni pamoja na kuondoa uwezekano wa Mtu kujiandikisha mara mbili (double registrations) katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Kwa kutumia teknolojia ya BVR Mpiga Kura ataweza kutambuliwa iwapo tayari alikwisha kujiandikisha pale tu atakapoweka vidole kwenye mashine ya Utambuzi yaani finger printer.

Narudia kusisitiza kuwa Mfumo wa BVR utaweza kutoa majibu kwenye changamoto ambazo zilijitokeza wakati wa matumizi ya mifumo mingine iliyotangulia kama vile Kuondoa Wapiga Kura waliojiandikisha zaidi ya mara moja, Kutambua Wapiga Kura siku ya uchaguzi na Kuhamisha kwa urahisi majina ya Wapiga Kura watakaohitaji kurekebisha taarifa zao kutokana na kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Ndugu zangu Wanahabari.

Tume inapenda kusisitiza kuwa zoezi hili lilikuwa la majaribio. Kufanyika kwa zoezi hilo kumeiwezesha Tume kubaini changamoto mbalimbali zikiwemo zile nilizozitaja hapo awali na hivyo kutoa fursa sasa kwa Tume kuzifanyia kazi na kuhakikisha kuwa lile zoezi kubwa litakalofuatia linafanyika kwa ufanisi zaidi.

Matumizi ya BVR katika Uandikishaji wa Wapiga Kura yanatumika hapa nchini kwa mara ya kwanza hivyo kwa namna yoyote changamoto ni lazima zijitokeze. Lengo kuu la mradi wa majaribio lilikuwa ni pamoja na kuiwezesha Tume kubaini changamoto hizo na kuzipatia ufumbuzi.

Napenda nisisitize pia kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi inayo dhamira ya dhati ya kukuza demokrasia kwa kuandaa na kuendesha chaguzi zake katika mazingira rafiki na wazi yatakayotoa fursa kwa kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 kutumia haki yake ya kikatiba ya kuchagua viongozi wake. Tume itakuwa tayari kupokea maoni na ushauri kutoka kwa wadau mbalimbali wa Uchaguzi kuhusu namna bora ya kufanikisha majukumu yake. Aidha Tume itaendelea kubuni mbinu na mikakati itakayoboresha utendaji kazi wake.

Ndugu Waandishi wa Habari,

Kwa kumalizia, ninapenda tena kuwashukuru wote kwa kuhudhuria Mkutano huu. Tume mara zote imekuwa ikitambua mchango wa Vyombo vya Habari katika kufikisha ujumbe kwa jamii inayokusudiwa. Hali kadhalika katika zoezi hili la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa kutumia BVR vyombo vya habari vimekuwa mstari wa mbele katika kuufahamisha umma wa watanzania na kuhamasisha wale wote

wenye sifa kujitokeza na kujiandikisha. Tume inatambua na kuthamini mchango wenu huo.

Kwa mantiki hiyo niendelee kutoa rai kwenu na Wadau wengine wa Uchaguzi kutoa taarifa zilizo sahihi na kuhamasisha Wananchi kushiriki katika zoezi hilo kubwa linalotarajia kuanza wakati wowote kuanzia sasa. Ni mategemeo ya Tume kuwa kwa kupitia kalamu na vipaza sauti vyenu taarifa hizi zitawafikia Wapiga Kura wetu na hatimaye wataweza kujitokeza kwa wingi na kujiandikisha pindi muda huo utakapowadia.

ASANTENI KWA KUNISIKILIZA